



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA**



HALMASHAURI YA ROMBO

Kumb. Na.

29/06/2022

RUDIO LA TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Kwa mara nyingine Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo anayo furaha kutangaza nafasi **mbili (2)** za ajira ya kudumu kwa watanzania wote wenye sifa stahiki za kujaza nafasi hizo **Katibu Muhtasi Daraja la III**.

KATIBU MUHTASI DARAJA LA III NAFASI MBILI (2).

1. SIFA ZA MWOMBAJI

- Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne waliohudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu.
- Wawe wamefaulu somo la hatimkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambulika na Serikali na kupata cheti katika program za windows, Microsoft office, Internet, E-Mail na publisher.

2. MAJUKUMU YA KAZI

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutuma taarifa, kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanyia kazi na kumwarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

3. MSHAHARA.


- Cheo cha **Katibu Muhtasi daraja la III** kina Mshahara wa **TGS B1** kwa mwezi

MASHARITI YA JUMLA:

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wawe na umri kati ya miaka 18 hadi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.

- III Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya
- IV Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali:
- Cheti cha Taaluma husika
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV au VI
 - Cheti cha Astashahada ya Uhazili
 - Cheti cha kompyuta
 - Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- V. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- VI. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 12/07/2022 saa 9:30 Alasiri.
- VII. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo.

Mkurugenzi wa Halmashauri,
Halmashauri ya Wilaya ya Rombo,
S.L.P.52,
Mkuu-Rombo.



Godwin Chacha

**MKURUGENZI MTENDAJI (HW),
ROMBO**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
ROMBO**